Kikao cha Saba – Tarehe 21 Oktoba, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 96

Ukosefu wa Gari kwa Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mhe. Mohammed Said Mohammed) – Aliuliza:-

Itakumbukwa kwamba, Ofisi ya Waziri Kiongozi ya Awamu ya Sita iliagiza gari ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itumiwe na Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu. Hata hivyo, bado gari hiyo inatumiwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto huku bodi inaendelea kuwa na upungufu wa gari kwa shughuli zake.

(a) Je, kwa nini agizo hili halikutekelezwa kama ilivyoagizwa?

(b) Kwa kuwa Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa gari, serikali haioni kuwa gari hiyo ingekabidhiwa kwa bodi hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 96 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imefuatilia agizo la gari ya Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu, ambalo Mhe. Mjumbe ameulizia. Lakini haikuona kumbukumbu zozote na wala haijapata taarifa juu ya agizo hilo. Aidha ofisi yangu imejaribu kuwasiliana na taasisi zote alizozitaja Mhe. Mjumbe, lakini taasisi hizo bado hazijaleta taarifa juu ya agizo hilo.

Kwa hivyo, tutaendelea kuwasiliana na Mhe. Mwakilishi, ili atupe taarifa za ziada juu ya suala hili, ili tuweze kufuatilia zaidi kwa nia ya kupata ufumbuzi wa suala hili wa gari ya Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu.

Nam. 84

Usafiri Baina ya Pemba, Unguja pamoja na Tanga

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Baada ya ajali mbaya ya Meli ya *MV. Spice Islander I* kusababisha maafa makubwa hapo tarehe 10/09/2011, meli nyingine inayosafirisha abiria bina ya Unguja na Pemba MV. Serengeti, mnamo tarehe 22/09/2011 mashine zake zilikataa kuwaka baada ya kupakia abiria kwa ajili ya kuwapeleka Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa meli ya MV. Serengeti haifai kwa kubebea abiria hadi itakapofanyiwa matengenezo makubwa?

(b) Mhe. Waziri, ni lini Unguja na Pemba utapatikana usafiri wa uhakika?

(c) Hii Idara ya Udhibiti wa Usafiri wa Vyombo vya Baharini kwa hapa Zanzibar ipo wapi na inafanya kazi gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 84 kama ifuatavyo:-

(a) Meli ya MV. Serengeti inafaa kubeba abiria, hata hivyo meli hiyo imezuiliwa kufanya safari zake za kawaida, kutokana na kuwa na kasoro ndogo ndogo zilizoonekana kwenye ukaguzi, ambazo hazihatarishi usalama pindi zikiondolewa. Kwa hivyo, meli hiyo itarejea katika safari zake za kawaida mara tu kasoro hizo zitakaporekebishwa na kuthibitishwa na Mkaguzi Mkuu wa Meli.

(b) Mhe. Spika, kuhusu suala la ununuzi wa meli mpya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ikishirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zimeagizwa na serikali kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya. Aidha wizara hizi zinaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali, ili kuangalia uwezekano kuekeza katika kupata meli mpya kwa ajili ya ubia au mkopo.

Hivyo, hadi sasa wizara hizi zimekutana na makampuni mbali mbali kwa ajili ya kutatufa ufumbuzi wa tatizo hilo. Miongoni mwa kampuni hizo ni hizi zifuatazo:-

- Kampuni ya. *Sudan Farmal International* kutoka Sudan;
- Kampuni ya *YDA* kutoka Turkey;
- Kampuni ya *ORIZONTE* kutoka Turkey;
- Kampuni ya *AL-YOUSEIF Charitable Society* kutoka. Saudi Arabia na
- Kampuni ya *DIMONIOS* inayotoka Uholanzi.

Mapendekezo yaliyotolewa na kampuni hizo yamepokelewa na yanafanyiwakazi na serikali

(c) Udhibiti wa usafiri baharini uko chini ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini, mamlaka hiyo iko katika jengo lililokuwa likitumiwa na Bohari Kuu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kazi zake kubwa kwa ujumla ni kusimamia shughuli zinazohusu usalama wa usafiri baharini hapa Zanzibar.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wizara ndio inayomiliki Shirika hili la Meli na taarifa tuliyonayo hapa Barazani kwamba Meli ya MV. Mapinduzi iliuzwa na fedha zile ilikabidhiwa serikali. *(Makofi)*

(a) Je, huoni kwamba fedha zile ilikuwa ndio chanzo cha kuanza kutafuta hiyo meli nyengine kwa sababu ni fedha za shirika, kwa nini serikali imezizuia na ikawa haikufanya utaratibu wa kununua meli?

(b) Kwa kuwa shirika hili bado lipo na kila mara tunapotaja kwamba livunjwe serikali bado ina kigugumizi katika kulivunja shirika hili. Sasa kwa nini hawapewi hiyo meli na ikawa lipo kweli hilo shirika badala ya kubaki shirika hewa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika,

(a) Ni kweli kwamba Shirika la Meli lilikuwa likiratibu na kuendesha meli ya MV. Mapinduzi na meli hiyo imeuzwa na serikali. Kwa kutambua kwamba meli hiyo ilikuwa chini ya umilikiwa wa Wizara ya Fedha kama ni msimamizi mkuu wa mali za serikali na fedha hizo bado ziko serikalini.

Kwa kweli kama tulivyoeleza katika majibu ya swali mama, kwamba Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zimetakiwa kushirikiana katika kutafuta wafadhili pamoja na makampuni, ili kuweza kupatikana kwa meli hiyo.

Kwa hivyo, ni imani yangu kuwa fedha hizo zilizoko Wizara ya Fedha bado ziko katika eneo ambalo, kwa sababu wizara hizi zinashirikiana na malengo ni kutafuta meli, basi sio kama kuna ulazima fedha hizo zirejeshwe katika Shirika la Meli, kwani malengo ni kutafuta meli mpya na wizara zote mbili zimetakiwa kushirikiana katika upatikanaji wa meli hiyo.

(b) Mategemeo yetu ni kwamba tutakapoweza kununua meli hizi mpya, basi zitaendelea kuwa chini ya usimamizi wa shirika baada ya kulifanyia marekebisho makubwa shirika hili na kuwa na nguvu zaidi za kisheria.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Inasemekana Meli ya MV. Sengereti chini imetiwa zege. Kwa kuwa majuzi tu tulitokewa na ajali ya Meli ya *MV. Spice Islanders I*. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba suala hili linahatarisha maisha ya Wazanzibari wote? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, anachokisema Mhe. Mjumbe, ni uvumi na wala si jambo jema kwa kiongozi kama yeye kukamata uvumi hivyo ni vizuri anayoyasema kuyafanyia uthibitisho. Kutokana na hali hiyo, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba meli hiyo ya Serengeti haina zege kama watu wanyosema tena meli hiyo imo salama kwa msingi huo wa zege na mamlaka husika imeizuia meli hiyo kwa mapungufu mengine.

Lakini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kuondoa shaka hiyo kama ilivyotoa maelekezo na kamati husika, tunaendelea kufanya mawasiliano na wenzetu wa *SUMATRA* na mategemeo muda wowote watakuja hawa kwa ajili ya kushirikiana nami katika kufanya uchunguzi wa kuvihakiki vyombo vyote vinavyofanya safari za usafiri kati ya Unguja na Pemba.

TAARIFA

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, nimwambia Mhe. Waziri inasemekana na wala sina uhakika, hivyo asiniambie kuchukua uvumi kwa Mwakilishi kama mimi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, kwa hivyo nafikiri majibu yamekwenda sambamba, kwa sababu Mhe. Mjumbe anasema inasemekana na Mhe. Naibu Waziri anasema hiyo haina. Kwa hivyo, huo ni uvumi tu unaosemekana nje na wala haina tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kuwa katika hali ya afya. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa maelezo yake kwenye swali mama ni kwamba serikali iko mbioni kwa ajili ya kununua meli. *(Makofi)*

(a) Je, Mhe. Waziri haoni kama hivi sasa kuna haja serikali hizo mbio zikawa za *marathon*, kwa kuhakikisha kuwa inajikita kununua meli hiyo? *(Makofi)*

(b) Kutokana na fedha zilizouzwa meli ya MV. Mapinduzi pamoja na fedha zilizochangwa kwa ajili ya ajali ya meli ya *MV. Spice Islander I* zikachanganywa, kwa lengo la kununuliwa meli haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza napenda nimwambie sana mama yangu kwamba dhamira ya serikali ni kununua meli, pia ninamuomba aingie katika kundi la kwanza la kuamini wale wenye kuamini kwa kusikia na wala asiingie kwenye kundi la pili la wenye kusubiri kuamini kwa kuona.

(a) Mategemeo ya serikali ni kwamba malengo ya serikali inaposema kununua meli kuna tofauti na kununua vifaa vyengine, kwa sababu lazima kuna muda utapita usiopungua miezi kumbi na mbili kwenda juu katika matayarisho ya kununua meli. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mjumbe ajenge imani na serikali, kwani malengo ya serikali ni kununua meli na serikali imedhamiria kwa dhati kufanikisha jambo hili.

(b) Mawazo haya ya kuchanganya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maafa yatokanayo na meli ya *MV. Spice Islander I* na zile fedha zilizopatikana baada ya kuuzwa Meli ya MV. Mapinduzi, nadhani serikali ipo tena ni sikivu, basi itayachukua na kuyafanyiakazi kwa mujibu wa maslahi.

Lakini imani yangu ni kwamba fedha hizi kwa ajili ya meli ya *MV. Spice Islander I* zinazo matumizi na utaratibu wake kama ulivyoelekezwa na serikali. Malengo ya serikali ni kutafuta fedha kwa ajili ya kufanikisha ununuzi wa meli kama ilivyoelezwa na vyombo husika. *(Makofi)*

Nam. 74

Zoezi la Kuratibu Vitambulisho vya Taifa

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakamilisha zoezi la kuratibu na kutoa Vitambulisho vya Taifa, ambavyo vinatarajiwa kutolewa muda mfupi ujao.

(a) Je, vitambulisho hivyo vina uhusiano gani na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi?

(b) Je, serikali imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi, ili wajuwe umuhimu wa vitambulisho hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 74 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika kufanyakazi Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inashirikiana kwa karibu na Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanikisha utoaji wa vitambulisho hivyo kwa upande wa Zanzibar.

Hata hivyo, vitambulisho vitakavyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka hiyo ya Vitambulisho vya Taifa vitakuwa ni Vitambulisho vya Uraia na vitatolewa kwa raia wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuwepo kwa vitambulisho hivyo hakutaathiri hata kidogo wala

kubadilisha utaratibu uliopo hivi sasa wa kutoa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

(b) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeanza kutoa elimu kwa wananchi kupitia makundi mbali mbali. Hata hivyo, Afisi yetu ya Usajili na Kadi za Utambulisho kwa kupitia kipindi chake cha redio kinachorushwa hewani kila wiki kupitia Shirika la Utangaza la Zanzibar, imekuwa ikitoa elimu na ufafanuzi wa kina juu ya suala hili.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri atakubalaina nami kwamba suala la uraia hususan Tanzania Bara lina utata kwa sababu nchi yetu imezungukwa na mipaka na watu wameingia nchini kwa muda mrefu.

Suala hili lina ushahidi kwa baadhi ya watu au wananchi kufikia hata hatua ya kugombea uongozi, lakini dakika za mwisho anaambiwa uraia wake una utata na kuenguliwa katika nafasi hizo.

Je, ni vigezo gani vitakavyotumika kujua Utanzania au uraia wake mtu?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ukweli kwamba hakuna utata wala tatizo lolote, isipokuwa watu kwa zile taratibu zilizowekwa hawazifuati, kwa sababu taratibu zimewekwa na zimeelezwa wazi.

Kwa mfano, mtu ili kuwa raia wa Tanzania ni wa namna gani, pia na mtu anayetaka uraia wa Tanzania afuate taratibu gani. Kwa hivyo, mambo yako wazi na kama nilivyosema kwamba elimu hii inatolewa katika kipindi cha redio kinachotolewa kila wiki kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar.

Kwa hiyo, kama kuna utata wowote na mimi mwenyewe nimeone kwenye magazeti wale watu wanaoomba uraia wa Tanzania. Kwa mfano, wanaomba *Passport*, kwanza wanajitangaza kwenye magazeti ikiwa kuna mtu mwenyewe pingamizi, basi anatoa pingamizi. Nafikiri suala la msingi ni kufuata taratibu zinazowekwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa mujibu ninavyofahamu ni kwa zaidi ya Kitambulisho hiki cha Uraia cha Utaifa cha Tanzania, basi kutakuwa na Vitambulisho vyengine vya Ukaazi na kadhalika kutokana na kila mtu na mazingira yake katika hii Tanzania.

Lakini wakati huo na sisi Wazanzibari tunacho kitambulisho chetu, ambacho kinaitwa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kwa vile hakuna Kitambulisho cha Uraia cha Mtanzania Mkaazi.

Je, haionekani kwa sababu nchi hizi ni mbili na kila moja inayo mambo yake ya kiuendeshaji na sisi kikawa kitambulisho kwa maana ya kuwa ni cha Mzanzibari na hili

neno Mkaazi liondoke, ili tusije tukaona kuwa kitambulisho chetu ni *subordinate* ya Kitambulisho cha Utaifa wakati Zanzibar nayo ni nchi?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nafikiri wakati nilipokuwa nikijibu swali langu la msingi nilisema tofauti ya vitambulisho hivi viwili. Kwa kweli tofauti iko wazi kabisa kwamba hiki kimoja ni Kitambulisho cha Uraia wa Watanzania na hiki chengine ni Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, yaani tofauti iko wazi.

Sasa kama tunazungumzia watatokea Watanzania Wakaazi, basi tusubiri ofisi itakuja kuweka utaratibu na kupambanua wakati huo ikianza kazi. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri amesema kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ya Tanzania itashirikiana na Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutoa Kadi hizi za Uraia.

Mhe. Spika, katika semina iliyopita miezi michache iliyopita nyuma tuliambiwa wazi kwamba Afisi ya Mambo ya Ndani itachukua kumbukumbu zote za Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na kuziingiza kwenye Vitambulisho vya Uraia. Sasa kwa kuwa hadi hii leo Wazanzibari wengi bado hawajapata Vitambulisho vya Ukaazi.

(a) Hivi Mhe. Waziri anakusudia kuniambia kwamba wale ambao hawana vitambulisho ndio watakosa uraia na kama watakosa uraia basi tuwapeleke raia wanchi gani?

(b) Mhe. Spika, naomba kujua tofauti ya *Passport* na Uraia na

(c) Ibara ya 11 ya Katiba ya Zanzibar inazungumzia usawa wa binadamu, ibara ya 12 usawa mbele ya sheria na ibara ya 6 nani Mzanzibari. Sasa iwapo Katiba hii haiwatendei haki Wazanzibari, ambao hawajapata Vitambulisho vyao vya Ukaazi. Je, ni kusema kwamba SMZ inavunja Katiba?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba nilisema kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inafanyakazi zake kwa kushirikiana karibu sana na Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Ni kweli kuwa kwa kuanzia watatumia *Database* hii walionayo Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ya Zanzibar, lakini hawatoishia hapo kwa sababu wao wanayo mipango ya kufungua afisi kila wilaya.

Hivyo, hivi sasa tayari Afisi zetu za Wakuu wa Mikoa na Wilaya wameshaombwa watafute maeneo kila wilaya, kuweza kupata sehemu ya kujenga afisi tena afisi hizo zitakuwa wazi na zitajengwa pia zitakuwa huru kabisa kwa kila Mtanzania mwenye sifa za kuzaliwa au nyenginezo za kupata uraia wa Tanzania, basi atakuwa na haki ya kupata huo uraia wa Tanzania.

(b) Kuhusu tofauti ya *Passport* na Uraia. Mhe. Spika, nafikiri iko wazi, yaani hili ni neno la Kizungu kabisa *Passport* ni cheti cha kusafiria au haki na hii ni uraia, tena ni vitu viwili tofauti na wala tusivichanganye.

Lakini sasa kuipata *Passport* ya Tanzania ni lazima uwe Mtanzania na wala mtu hawezi kuwa nchi za nje na kuchukua *Passport* ya Tanzania. Kwa hivyo, hivi sasa kuna maombi yametokezea kwamba tuweke *dual*, yaani watu wachukua *Passport* zaidi ya moja.

Jambo hilo nimesikia Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania nimesikia kwenye vyombo vya habari na hata Mhe. Waziri mwenyewe wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwamba litazingatiwa na serikali.

(c) Suala la Vitambulisho kwamba kuna watu bado hawajapatiwa vitambulisho, jambo hilo tayari tumeshasema mara nyingi kwamba hii ni haki ya kila Mzanzibari kupata Kitambulisho cha Ukaazi. Lakini suala la msingi afuate taratibu zilizowekwa na wala haiwezekani mtu kama hajatimiza masharti yaliyowekwa tena aombe kitambulisho apate. Sasa ikiwa mtu amefuata taratibu zilizopo basi hakuna tatizo lolote ni haki yake na tutahakikisha kwamba wanapatiwa.

Nam. 67

Wanafunzi Wanaomaliza Darasa la Kumi (*Form II*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali imeweka Elimu ya Lazima kuanzia darasa la kwanza hadi la kumi kwa watoto wote wa Kizanzibari, ili kudumisha dhamira ya Mapinduzi matukufu ya 1964 pamoja na kuwawezesha watoto wa wakulima na wananchi wote kwa ujumla kufaidika na elimu nchini.

(a) Je, serikali haioni kwamba masomo ya lazima kumalizika Darasa la Kumi (*Form II*), kunawakosesha watoto wetu wa wakulima kukosa elimu ya juu?

(b) Kwa kuwa wanafunzi wanaomaliza Darasa la Kumi (*Form II*) ni watoto wa wakulima na kwa kuwa wazee wao wanashindwa kuwasomesha na kuwaendeleza katika Skuli za Watu Binafsi. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watoto hao?

(c) Pamoja na hatua nyengine inazopasa kuzichukua. Je, serikali haioni kwamba inapaswa kudhibiti gharama za masomo katika Skuli za Watu Binafsi, ili watoto wetu waweze kupata elimu katika skuli hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 67 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa imekuwa ni dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa Elimu ya Lazima kwa watoto wetu wa Zanzibar, ili wote waweze kufaidika na upatikanaji wa elimu hapa nchini. Kwa muda mrefu Elimu ya Lazima imekuwa ikitolewa kwa miaka 10, kuanzia darasa la kwanza hadi l a kumi (*Form II*).

Hata hivyo, katika Sera ya Elimu ya mwaka 2006 iliagiza Elimu ya Lazima itolewe kwa muda wa miaka 12, yaani kuanzia miaka miwili ya Maandalizi, miaka 6 ya Msingi pamoja na miaka minne ya Elimu ya Sekondari hadi kidato cha nne.

Utekelezaji wa sera hii unafanyika hatua kwa hatua ndio maana serikali imeweka mkazo katika kupanua Elimu ya Maandalizi. Mhe. Spika, wakati huo huo kupanua upatikanaji wa Elimu ya Sekondari kwa kujenga skuli mpya, ili wanafunzi wengi zaidi waweze kupata nafasi na kufika hadi kidato cha nne.

Baada ya maelezo haya napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali imekubali kuwa wanafunzi wetu kumaliza Elimu ya Lazima hadi kidato cha pili haitoshi. Kwa kweli mahitaji ya elimu katika karne ya 21 na ndio maana ikapitishwa Sera mpya ya Elimu ya mwaka 2006, ambapo Elimu ya Lazima itaongezwa hatua kwa hatua na hatimaye wanafunzi wote kufikia hadi kidato cha nne.

(b) Wanafunzi wengi wanaomaliza masomo ya Elimu ya Lazima katika kidato cha pili wanajiunga na Skuli Binafsi au Madarasa ya Kujiendeleza, ambayo yameenea katika sehemu mbali mbali ya nchi yetu. Madarasa ya Kujiendeleza ambayo yamo katika skuli zetu nyingi za sekondari ni ya gharama nafuu tena wanafunzi wengi wanaweza kujiendeleza.

(c) Wizara yangu inadhibiti ada zinazotozwa na Skuli Binafsi na hadi sasa ada zinazotozwa zinalingana na huduma zinazotolewa na wananchi wengi wameweza kumudu kusomesha watoto wao katika skuli hizo.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Wizara yake imeanzisha Sera mpya ya Elimu ya kwamba wanafunzi wote waanzie Elimu ya Msingi hadi darasa la kumi na mbili.

Je, umefikia hatua gani kwa hilo na lini hasa utaweza kuitekeleza sera hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mhe. Mwakilishi kwamba tumepitisha Sera mpya hapa ya mwaka 2006 ya Elimu ya Lazima ni kuanzia *Nursery* mpaka darasa la kumi na mbili (*Form IV*).

Mhe. Spika, tukitizama kwenye MKUZA tumeeleza pale kwamba ukifika mwaka 2015, basi *Nursery Schools* zetu ziwe tayari zimefikia asilimia 50. kwa hivyo, asilimia 50 ya wanafunzi wetu watakuwa tayari wameanza kupata elimu ya *Nursery* ya miaka miwili

Lakini Mheshimiwa tukienda kwenye bajeti yetu pia tumeeleza hatua ambazo tunakwenda mwaka hadi mwaka, kwa mfano mwaka uliopita tumeweza kupitisha watoto kufoka Form II mpaka Form III na Form IV kwa asilimia karibu 54.2% kwa mwaka 2009 na kwa mwaka 2010 tumefikia asilimia 58% itaonekana ni nama gani ambavyo elimu hii tumeitanua na kufuata sera yetu hatua kwa hatua, si rahisi moja kwa moja kutoa sera na kuweza kuitekeleza kama ilivyo kutokana na hali halisi tunahitaji walimu, lakini majengo ambayo tunayo ya skuli za sekondari hayatoshi.

Kwa hivyo hapa tuna Skuli 21 za sekondari za kisasa ambazo Mhe. Spika, mara nyingi nimekuwa nikizitolea kauli hapa na ishaalla kifika mwakani skuli 13 tutazifungua na tutakuwa na walimu wengine ambao wanarudi vyuoni, kwa hivyo kwa mafanikio haya Mheshimiwa tutaweza pia kuzidisha idadi ya watoto ambao wataingia darasa la kumi (10) mpaka la kumi na mbili (12).

Kwa hivyo tunakwenda hatua kwa hatua.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Katika kunyanyua elimu ya watoto wetu wazazi pamoja na walimu wamejitahidi kufungua skuli za ziada yaani *tuition* ili kuendeleza watoto wetu.

Je, ni utaratibu gani ambao huchukuliwa katika kufunguliwa hizo *tuition* na Wizara huongeza bidii gani au msaada gani katika kuendeleza watoto wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaruhusu masomo ya ziada kwa ajili ya watoto wetu kujiendeleza umaarufu *tuition*, utaratibu upo skuli yoyote ambayo inataka kufungua *tuition* basi ni lazima iiandikie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na Wizara inachukua hatua ya kuhakikisha kama skuli husika imewasiliana na kamati ya Skuli, tukiridhika kama skuli husika ambayo inataka kufungua *tuition* imewasilana na kamati ya skuli basi ruhusa hiyo hutolewa.

Lakini vile vile Mhe. Spika, kuna hizi kambi na hivi sasa zimezua maneno mengi pamoja na *tuition* nataka niseme kwamba kambi zilizoanzishwa zipo kisheria Mhe. Spika, nazo hutolewa maombi hivyo hivyo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wizara ikirizika kama sehemu huzika inayotaka kufunguliwa kambi iko salama na sio kama ipo salama tu, lakini ina walimu ambao ni walimu wetu na ina ulinzi ambao utafaa kwa ajili ya kulinda watoto wetu basi pale kibali hutolewa.

Lakini nichukue fursa hii kuwaomba wazazi wizara ilitoa tamko kuwa *tuition* ni kuanzia jioni mpaka saa 2.00 usiku, kwa hivyo tamko lile lipo pale pale naomba wazazi washirikiane na walimu wetu na vituo hivi vya *tuition* kuhakikisha mtoto wake ikifika saa 2.15 hajarudi nyumbani basi amuulize alikuwepo wapi. Kwa sababu tumeona vituo hivi sasa vinaleta matatizo badala ya kunyanyua elimu ya mtoto sasa tunapata wajukuu Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe,. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa mafanikio ya mpango au sera yoyote nzuri katika elimu yanapaswa yaonekane katika kiwango cha uwezo wa kupasisha wanafunzi, kwa sababu skuli za Zanzibar muda mrefu zimekuwa zikishika mkia katika matokeo ya Taifa katika Tanzania na kufanya vibaya sana mwaka jana.

Je, Wizara ya Elimu inapimaja mafanikio ya sera yake ya elimu ?.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwama mafanikio ambayo unaweza kusema umefanikiwa ni kupima upatishaji wa watoto, lakini niseme licha kuona kwa macho ya kawaida kama elimu ya watoto wetu inashuka mimi nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu, kwamba elimu ya watoto wetu bado haijashuka kwa kiasi hicho ambacho tunafikiria na ndio maana kila mwaka tunakuwa na wimbi kubwa la wanafunzi ambao wanaomba kwenda kusoma katika elimu ya Juu Mhe. Spika.

Nam. 46

Chumba cha Upasuaji Theatre

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Katika Chumba cha upasuaji cha Hospitali ya Mnazimmoja *“air-conditioner” (AC)* hazifanyikazi kwa kipindi kirefu na kwa kuwa “air conditioner” hizo ni muhimu katika chumba hicho ili kazi za upasuaji zifanyike vizuri.

Ni lini AC hizo zitatengenezwa ili huduma ya upasuaji ziendelee bila ya usumbufu.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, huduma za upasuaji katika hospitali ya Mnazi Mmoja hazijasita zinaendelea kama kawaida na hivi sasa kuna kambi za Madaktari kutoka Spain wanaendelea na *Operation* za Vichwa Maji na Uti wa Mgongo *(Neuro surgery).*

Mhe. Spika, *Air Condition* za vyumba vya upasuaji zinafanyakazi saa 24 zikiwemo operesheni za kawaida na za dharura. Kwa vile *AC* ni kifaa ambacho kinatumika muda wote kinahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Ni *AC* moja tu ambalo haifanyi kazi kabisa nalo liko varanda ambako kumewekwa mafeni mawili mapya kwa kupitia ufadhili wa *Zanzibar Outreach Program (ZOP).*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Pamoja na taaluma wanayohitaji madaktari wetu wa upasuaji lakini vile vile huhitaji mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwa ni moja ya kuwepo kwa kiyoyozi cha kuweza kutoa ubaridi wa kutuliza mawazo yao pale.

a) Je, kwa kuendelea kuifanyia matengenezo *AC* moja sio kununua mpya lakini kuifanyia matengenezo jambo ambalo linapelekea kupoteza ufanisi kwa madaktari wetu wazuri. Je, si kuhatarisha maisha ya wagonjwa wetu.

b) Kwa kuwa Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja dhamira ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuifanya kuwa Hospitali ya Rufaa. Jee kitendo cha kuendelea kuweka ma- *AC* mabovu na kuyatengeneza mara kwa mara si kucheleweshe dhamira halisi ya serikali yetu ya kuifanya hospiteli hii kuwa ya rufaa.

Mhe. Waziri wa Afya: Nakubaliana nawe kabisa kwamba madaktari wetu wanahitaji mazingira mazuri ya kufanya kazi pamoja na viyoyozi, lakini nafikiri Mheshimiwa utanikubalia hata mumu umeme huzimika na viyoyozi vikaharibika, hilo ni jambo la kawaida na kutengeneza ma- *AC* hayo tutashughulikia kama inavyostahiki.

Juzi nilipokuwa najibu hapa nilisema kwamba kuna mpango na mradi mkubwa wa kufanya masahihisho ya hospitali ya Mnazi Mmoja chini ya mradi wa *Oriol*, na masuala yote ya kutengeneza hospitali ile ikawa na sura nzuri umeshakamilika na unaanza kutekelezwa mwaka unaofuata.

Sasa haya ya kuharibika mara kwa mara ni sehemu ya kawaida na vile vile ni kutokana na ufinyu wa bajeti yenyewe, hatujasahau juzi Mhe. Omar Yussuf alisema hapa kwamba kipindi cha Julai, Septemba cha bajeti ya serikali kinakuwa kigumu huwa kuna ufinyu wa kupata mapato, na sisi si kisiwa mbali na serikali hii sisi ni sehemu ya Wizara za Serikali

na maombi yetu yanabiti yatoke huko huko Wizara ya Fedha, tunapotiliwa fedha tunafanya lile lililo muhimu zaidi kutengeneza na hili tutalitengeneza kama tunavyotengeneza vitu vyengine na ikilazimu tutalitia jipya.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa ninavyokumbuka mimi Wizara ya Afya inacho kitengo cha ufundi na matengenezo kama haya wenyewe wanaziita *m routine maintenance* je hotokezeaji mpaka mtu wa nje akanda kuona kwamba kifaa ni kibovu, na hali hiyo inaendelea na kitengo kipo. Mhe. Waziri ana maelezo gani ya ziada ya kutueleza.

Mhe. Waziri wa Afya: Nakushukuru kwamba umenisaidia kunikumbusha kwamba tuna kitengo kizuri sana na kina ma - *engineer* ambao wanafanya *routine maintance* lakini leo unapokuja kulikuta feni bovu ikawa ni hoja kesho unaweza kulikuta zima, sasa siku aliyopita Mheshimiwa huyu lilikuwe *Air condition* bovu haina maana kwamba hatutengenezi, nimesema hapa haya ni mambo ya kawaida kwa hivyo kitengo chetu kinafanya kazi tena kinafanya vizuri sana na tunaendelea kukiimarisha hata juzi tumeajiri ma- *engineer* wengine.

Nam. 70

Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Kariakoo

Mhe. Mohammed Said Mohammed - Aliuliza:

Kiwanja cha kufurahishia Watoto Kariakoo, kwa muda mrefu sasa kimekuwa hakitoi huduma yake iliyokusudiwa ya kuwafurahisha watoto wa Zanzibar, hali iliyosababisha viwanja vya Mnazimmoja na Forodhani kujaa sana.

(a) Kuna taarifa kwamba, kiwanja hicho kimekabidhiwa kwa ZSSF kwa ajili ya matengenezo. Je, ZSSF imepewa kiwanja hicho kwa mikataba ya aina gani na Je, matengenezo hayo yatakamilika lini.

(b) Kwa kuwa kila mwaka huwepo msongamano mkubwa wa watoto katika viwanja vya Mnazimmoja na Forodhani. Je, Serikali haioni kwamba kuchukua muda mrefu kwa matengenezo ya kiwanja cha Kariakoo na kutotumika kwake kunaweza kuhatarisha usalama wa watoto wetu katika siku za sikukuu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe naomba sana tuheshimu kanuni ya kuzima simu zetu ndani ya ukumbi huu, naomba sana tuheshimu kanuni hiyo na itabidi iwe tunaitekeleza ipasavyo kwa yule atakayevunja kanuni hiyo, ambayo ni kumtoa nje na kukosa posho la kikao.

Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kukosekana huduma katika kiwanja cha kufurahishia watoto cha Kariakoo kimeathiri viwanja vyengine ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la watoto katika viwanja vya Mnazi mmoja na Bustani ya Forodhani.

Kiwanja hicho cha Kariakoo Wizara yangu ni mlezi na tayari Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Wizara ya Fedha imekikabidhi kiwanja hicho kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ili kukifanyia marekebisho makubwa pamoja na kile cha Tibirinzi Pemba ili viweze kutoa fursa kwa watoto wetu kusherehekea Sikukuu mbali mbali.

(b) Mhe. Spika, kuchelewa kwa matengenezo ya kiwanja hicho ni kweli yanaweza kuleta athari na kuhatarisha usalama wa watoto katika viwanja vyengine, lakini Serikali imekuwa ikichukuwa juhudi za makusudi katika kulinda usalama wa watoto wetu. Imani yangu ni kwamba kuchelewa huko huenda ikawa ni matayarisho makubwa ya matengenezo ya kiwanja hicho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Waziri ni makubaliano gani au ya miaka mingapi waliyopewa ZSSF kwenye mikataba ambayo imetiwa na Wizara yako.

b) Kwa kuwa ZSSF imeelekea kushindwa na ujenzi wa kiwanja kile haioni haja ya Wizara kuipa taasisi nyengine ikakiendeleza kiwanja kile.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwanza nataka nimhakikishie kwamba Serikali na Serikali au Wizara na Wizara kunakuwa hakuna mikataba ya Wizara na Wizara, kwa sababu sote ni taasisi za serikali kwa hivyo hatuna mikataba hiyo.

Lakini la pili nataka nimwambie Mhe. Muwakilishi kwamba kile kiwanja ni mali ya serikali Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo walikabidhiwa kukisimamia, hali lipokuwa mbaya tuliwaomba wakirejeshe Hazina ambaye ndio mmiliki wa mali za Serikali na sisi tuwakabidhi ZSSF wakiendeleze.

Lakini la tatu napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kile kiwanja hakitafanyiwa ukarabati lakini kinajengwa upya michoro iko tayari, ZSSF fedha wameshaweka tayari tulikuwa tuna utata mmoja ndio maana tukachelewa, kulikuwa na mwenzetu mmoja pale alikuwa kapewa alichelewa kuondoka na ndio yale maduka mnayoyaona mle ndani wengine wanauza, wengine wanafanyaje sasa mmoja alichelewa kuondoka na ndio sababu na sisi tukachelewa kuanza.

Namuomba Mhe. Muwakilishi avute subira pale ndani kutakuwa na sehemu za kuchezea watoto, ndani kutakuwa na ukumbi wa mikutano na kutakuwa na sehemu ya kuegesha magari, tunataka kujenga uwanja wa kisasa na wa kileo kabisa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa viwanja hivi viwili vilitengwa na vilianza kutumika kwa ajili ya kufurahishia watoto hususan siku za mapumziko na sikukuu kwa jumla, kwa kuwa watoto ni sehemu ya jamii kwa nini kunakuwa na ukimya wa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu maendeleo ya viwanja hivi mpaka inafikia wakati watu wanakata tama.

b) Nimeshtuka kidogo katika suala la ziada alilojibu Mhe. Waziri wa Fedha, Mipango na Maendeleo kwamba kutakuwa na ukumbi wa mkutano, huu utakuwa ukumbi wa mkutano wa watoto au watu wazima. Kwa sababu ni kiwanja cha kufurahishia watoto sasa kidogo imenishtua kwa hivyo naomba jibu la nyongeza.

c) Kwa sababu kiwanja cha Kariakoo kuna mtu mmoja hajataka kuondoka je, ni lini tutaanza kuona ujenzi huo. Lakini kwa kuta Tibirinzi wamekabidhiwa hao hao lakini hakuna mtu mwenye chake je, tutegemee Januari kuanza Tibirinzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwanza hutoi tu taarifa kwa wananchi ambazo hazijakamilika, ukitoa taarifa kwa wananchi ambazo hazijakamilika utatoa matumaini ambayo kwa kweli *unnecessary* lakini kama taarifa zilizokamilika kwa wananchi tumewaeleza kwamba kiwanja cha Kariakoo ni kibovu na kimefungwa hiyo taarifa hiyo wananchi tumewapa.

Kwa hivyo namuambia Mhe. Muwakilishi kwamba taarifa inapokamilika ndio serikali hutoa kwa wananchi wake ili wananchi waweze kujua serikali inafanya nini.

Lakini la pili nataka nimwambia Mhe. Mwakilishi kwamba kiwanja hiki tumeona ni vyema kikawa kina huduma nyengine za ziada, kwa sababu eneo lile nalo ni kubwa ukumbi huo utakuwa wa mikutano sio mikutano ya watoto ni mikutano ya watu wote wanaotaka, kwa sababu watoto watakuwa wanachezea pale wakati wa jioni mikutano inaweza kufanywa wakati wa asubuhi ili kuweza kupata fedha za ziada.

Lakini nataka nimuongezee uwanja ule vile vile utakuwa na sehemu ya sinema hayo mambo yote kwa sababu ya kupata fedha kurudisha zile fedha za ZSSF kwa haraka zaidi na ufanisi zaidi. Tunataka kuutumia uwanja ule kuliko hata ulivyo hivi sasa.

Lakini vile vile amezungumzia kuhusu habari ya Tibirinzi nataka niseme kwamba lengo la serikali ni kulifanyia ukarabati au ujenzi mkubwa viwanja hivi, tutaangalia vile vile

suala la Tibirinzi tutakapokuwa tumemaliza Kariakoo tutakwenda na Tibirinzi tuombe dua tu fedha zipatikane ishaalla tutafanya shughuli hizo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa kiwanja cha Kariakoo pamoja na kusherehekea watoto wetu lakini ni pambo pia la mji wetu. Je, Mhe. Waziri kukiacha kiwanja kile na mibarika mikubwa kama msitu wa Ngezi sio kupoteza haiba ya mji wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mjumbe maelezo yote ameyaeleza waziri wa fedha kama tulivyoeleza mwanzo kwenye swali mama kwamba kiwanja hiki wizara yangu ni mlezi, sasa wakati Waziri wa Fedha ni mama na mimi ni mjukuu kiwanja kile tutajitahidi hakitokuwa na msitu kama ulivyosema umekuwa kama msitu wa ngezi, mama atakitayarisha vizuri na mimi mjukuu kwa kushirikiana nay eye.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini nataka nimhakikishie Waziri wa Fedha ni baba sio mama. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri kwa kuwa ulimi hauna mfupa.

Mhe. Spika: Nashukuru kwa taarifa na Mhe. Waziri ameipokea na nafikiri ameifahamu *(Kicheko)*

Nam. 57

Kisima cha Maji cha Kandwi

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Kazija Khamis Kona - Aliuliza:

Huduma ya maji kutoka Kisima cha Kandwi kwa sasa kinatoa huduma hiyo kwa wakaazi wa Pwani Mchangani Kubwa. Lakini huduma hiyo haiwafikii wakaazi wa Pwani Mchangani Ndogo.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako inayo taarifa hiyo.

(b) Kama unayo taarifa hiyo, ni hatua gani za haraka zimechukuliwa ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Pwani Mchangani ndogo.

(c) Wakaazi wa Pwani Mchangani Ndogo watarajie kuondokana na shida hiyo lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjiu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 57 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara yangu inaelewa kuwa wananchi wa Pwani Mchangani ndogo wanapata maji kupitia kisima cha Kandwi, ingawa upatikanaji huo si wa kuridhisha.

(b) Wizara yangu kupitia Mamlaka imechukua hatua za haraka za kuweka mgao maalumu kwa kuwaondoshea usumbufu wananchi hao.

(c) Ufumbuzi wa kudumu katika eneo hilo utapatlikana baada ya kukamilika mradi wa *ADB.*

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Ikiwa mradi huo wa *ADB* utawakamilishia watu wa Pwani Mchangani Je, wale wa Matemwe watakamilishiwa lini.

Mhe. Naibu Waziri Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba mradi wa *ADB* jimbo la Matemwe au pwani mchangani ni mjumuiko wa jimbo la Matemwe kwa hiyo wananchi wa Pwani Mchangani, wananchi wa matemwe wananchi wa Kandei, Kigomani wote watafaidika na mradi huo, baada tu utakapomalizika mradi huo. Wote watapata maji safi na salama.

Nam. 27

Ukosefu wa Ajiri kwa Vijana

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza -:

Pamoja na shauku kubwa kwa Serikali kuwapatia kazi vijana wa nchi hii, bado kuna tatizo kubwa kwa hizo kazi chache ziliopo kupewa vijana wanaotoka nje ya Zanzibar na hata nje ya Tanzania.

(a) Je, Serikali ina malengo au mpango gani ya kuona kwa zile kazi ambapo Wazanzibari wanaweza kuzifanya hazitolewi kwa vijana wa nje ya Zanzibar.

(b) Je, Serikali inaweza kutuambia ni lini mpango huo (kama upo) utaweza kutekelezwa na matokeo yake kuonekana kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 27 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, malengo makuu ya Wizara yangu ni kuhakikisha upatikanaji wa nafasi zaidi za ajira kwa vijana wa Kizanzibari il kuwapunguzia makali ya maisha. Katika kufanikisha azma hii, Wizara imeanza kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Inakusanya taarifa ya nafasi tupu za kazi kutoka taasisi mbali mbali na kuzitangaza ili vijana wenye sifa waweze kuomba

(ii) Imeanza utaratibu wa kuzungumza na wawekezaji/waajiri kwa lengo la kuwashajiisha watoe fursa zaidi kwa wazalendo pale zinapotokea nafasi za kazi;

(iii) Kupitia kitengo cha Taarifa za Ajira, wizara imeandaa mpango wa kukusanya taarifa za vijana wasio na kazi zitakazowezesha uandaaji wa mipango madhubuti ya ajira.

(iv) Wizara pia imepanga kutoa mafunzo mafupi kwa vijana ili kuwaandaa waweze kufanya vizuri wanapokwenda katika mahojiano ya kazi.

(b) Mpango huu unaendelea kutekelezwa na mafanikio yameanza kupatikana, ambapo baadhi ya waajiri wameanza kuwasilisha kwetu nafasi tupu za kazi walizonazo na Wizara huwa inazitangaza. Katika mwezi wa Julai – Septemba 2011, jumla ya vijana 15 wa Kizanzibari walinufaika na mpango huu kwa kupata ajira kwenye mahoteli. Aidha Wizara itaendelea kushirikiana na waajiri na washirika wengine katika kufanikisha upatikanaji wa ajira zaidi kwa vijana wa Kizanzibari.

Mhe. Ismaili Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa hatua alizozitaja zaidi zinalenga kuwapatia vijana kwa sasa lakini halirekebishi tatizo lilokuwepo. Na kwa sababu tayari hivi sasa kama alivyosema muuliza suala kuna vijana wengi ambao sio Wazanzibari ambao wanatumia nafasi ambazo kitaratibu zilipaswa kuwa ni za Wazanzibari. Na kwa sababu sheria zetu za kazi zinaeleza kazi gani ambazo hazipaswi kufanywa na wasiokuwa Wazanzibari. Wizara imejipanga vipi kuchukua hatua ya kufanya ukaguzi. Na kwa wale ambao wamechukua nafasi ambazo hawapaswi kuwa nao kuwaondosha ili Wazanzibari waweze kupata nafasi hizo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, wakati nafanya majumuisho ya bajeti yangu suala hili vile vile lilijitokeza. Nikalitolea ufafanuzi, lakini pia juzi nilipokuwa najibu suala kama hili nilitoa ufafanuzi juu ya hatua ambazo zinachukuliwa sasa hivi na kuhakikisha kwamba Wizara inapitia katika taasisi zote ikiwemo pamoja na mahoteli na kuona zile kazi ambazo zilihitaji kufanywa na Wazanzibari basi kuhakikisha kwamba kazi hizo wanapewa Wazanzibari. Na hata zile

ambazo kisheria haziwajibiki kupewa Wazanzibari lakini madamu shughuli hizo au taasisi hizo zipo hapa Zanzibar basi ni kuwapa kipaumbele Wazanzibari.

Napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na waheshimiwa wote kwamba hivi sasa kamishna wa kazi ameanza ziara maalum kutembelea katika taasisi hizo kuona maeneo hayo ambayo tunaweza tukawaweka wazalendo kufanya kazi hizo badala ya wageni.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara hii ina majina makubwa kazi, uwezeshaji wananchi, kiuchumi na ushirika. Na kwa kuwa ajira nyingi hupatikana katika sekta tatu, viwanda, uvuvi na kilimo cha kisasa.

Je, Wwzara yake inajishughulisha vipi kuhakikisha kwamba ajira hizi zinavutwa ndani ya nchi badala ya kutegemea hichi kilichopo tu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, suala la ajira na ukubwa wa wizara hii. Kwanza hii wizara jukumu lake ni kushirikiana na taasisi zote na sekta zote. Hii ni wizara mtambuka, wakulima wanahitajia kupata mafunzo kuelimishwa, baadaye tunahitajia kuwawezesha. Wavuvi wanahitajiwa kupatiwa mafunzo na baadaye tunahitajia kuwawezesha. Kwa hivyo ni jambo la kujenga mashirikiano mazuri. Tunahitaji kushirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wao vile vile ni wahusika katika suala, kushirikiana kwa pamoja. Kwa sababu ajira si lazima katika sekta hizo hata ajira za kujiajiri wenyewe kwa kuunda vikundi vya ushirika kama vile *SACOs* na vyenginevyo.

Mhe. Viwe Khamis Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Mhe. Waziri kuna vijana mbali mbali ambao wamejikusanya makundi katika kujitolea. Mfano *ZASOSEN.*

Je, wizara yako inampango gani kuwasaidia vijana kama hawa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, wizara yangu haiangalii kikundi cha aina ya *SAZOZE* tu inaangalia vikundi vya aina zote. Popote pale walipo tumejipanga kuwasaidia.

Nam. 54

Ufugaji wa Mbuzi

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza :-

Kwa kuwa wananchi wengi wamehamasika na kuanzisha au kujiunga na vikundi vya ufugaji wa Mbuzi wakiwa na lengo la kujikomboa kutokana na umasikini. Na kwa kuwa Mbuzi wanaotumiwa na wananchi hao kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa sio wale wa kisasa na maalumu kwa uzalishaji wa maziwa na huishia kutoa kiwango kidogo sana cha maziwa.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kuwatumia Mbuzi hao kunawazidishia wananchi wetu ugumu wa maisha kwa kutumia nguvu nyingi kufanya kazi isiyoleta tija.

(b) Ni lini hasa serikali itaweka bayana utaratibu wa kufuatwa kwa wananchi wote ili kupatiwa Mbuzi wa Kisasa wa Maziwa kupitia Mradi wa Kopa Mbuzi lipa Mbuzi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 54 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja.

Mhe. Spika, ni kweli wananchi wengi wamehamasika na kuanzisha au kujiunga na vikundi vya ufugaji wa mbuzi wakiwa na lengo la kujikomboa kutokana na umasikini baada ya kuona na kubaini kuwa mbuzi wanaotumiwa na wananchi wengi ni wale wa kisasa na wenye kutoa kiwango kikubwa cha maziwa, vyenginevyo wasingelihamasika.

Mhe. Spika, nikiri kwamba kuna baadhi ya wafugaji ambao hawafuati masharti ya kitaalamu katika ufugaji wao, ikiwemo mpango mzuri wa malisho, matumizi ya chakula cha ziada, utaratibu mzuri wa upandishaji na mbinu za ukamuaji maziwa. Ambayo hayo ni mambo yanayochangiya kuwa na uzalishaji mdogo au kutozalisha kabisa.

Hata hivyo, malalamiko ya Mhe. Mwakilishi tunayafanyia kazi, kwa kuimarisha elimu kwa wafugaji na utafiti wa mbuzi bora wa maziwa. Aidha naomba kutoa wito maalum kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wabunge na taasisi za dini, waanzishe mpango wa Majimbo yao au ya taasisi zao ya miradi ya kopa mbuzi lipa mbuzi angalau kwa kuanzia na mbuzi 30.

Ninahakika miradi hii ni rahisi kuanzia na itatoa umaskini kwa wananchi wa Majimbo yetu. Wizara yangu ikotayari kutoa ushauri kwa waheshimiwa na taasisi hizo, juu ya wapi mbuzi hao wanaweza kupatikana na vipi namna ya kuanzisha miradi hiyo na kuiendeleza kwa lengo lililokusudiwa.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri suala dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya yangu ya kusini ina mandhari nzuri ya ufugaji wa mbuzi. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kulishughulikia suala hili.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli Wilaya ya Kusini ina mandhari nzuri ya ufugaji wa mbuzi. Ndio maana kijiji cha Muungoni kilichopo jimbo la Muyuni Wilaya ya Kusini Unguja kikawa ni eneo la mfano katika ufugaji wa mbuzi. Wizara yangu inawasiliana na Shirika la Umoja wa Chakula (FAO) na tayari tumeshapeleka mradi maalum kwa ajili ya Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Micheweni.

Lakini pamoja na hayo Mheshimiwa Spika, wito niliotoa katika jibu mama kwamba sisi Wabunge na Wawakilishi tuone kwamba miradi hii tunaweza kuianzisha. Naomba tushirikiane na Wizara yangu ili kuwakomboa watu wetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa mujibu wa suala lilivyo ni kuwa wafugaji pamoja na kuwa wanakuwa na mbegu bora ya kiume lakini mbuzi wanaotumia ni wa kienyeji. Madhumuni ni kwamba wapate mbigu ambazo zitakuwa na maziwa mengi. Lakini kwa kuwa Mhe. Spika, mambo haya ni ya kubahatisha, wakati mwengine sifa ulizokusudia zinaweza zikenda kwa mtoto. Vyenginevyo inaweza ikatokea kinachozaliwa kikawa na sifa zile zile ambao kuwa ulikuwa huna haja nazo. Kazi ya ufugaji ni nzito sana hasa ufugaji wa mbuzi.

Je, Mhe. Waziri ni taaluma gani ya kweli aliyotumia na kuona kuwa wafugaji hawa wa mbuzi wanaohangaika sana watafaidika na kupata hizo sifa alizokusudia wakati kazi hii ya *cross breeding* tunasema ni ya kubahatisha.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, sio kweli kwamba ufugaji wa mbuzi ni kazi ngumu sana. Pale Muungoni Mhe. Spika, kina mama wazee sana ndio wanaoshughulika na kazi hii. Lamsingi ni kuhakikisha ushauri wa kitaalamu unaopewa unaufuata, bila shaka utapata matunda mazuri.

Sisi katika Wizara tunazo skuli za ufugaji 172 katika majimbo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo kupitia vituo hivyo Mhe. Spika, wafugaji wetu wakivutumia vizuri na wakifuata ushauri wa wataalamu uliotolewa pale kama ambavyo maeneo mengine. Mfano Kangagani kwa Pemba, kwa kweli ni maeneo ya mfano katika uzalishaji wa mbuzi na wanapata matunda mazuri.

Wito wangu Mhe. Spika, kwa wafugaji wote wa mbuzi, wazitumie skuli za ufugaji zilizopo, wafuate ushauri wa wataalamu, nina hakika matunda yao yatakuwa mazuri zaidi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa wataalamu wetu wamefanikiwa sana kuzalisha mbegu ya ng'ombe chotara ambazo hufaidika kupata faida kubwa kwa wafugaji wetu. Je. Mhe. Waziri ni lini wataalamu wa mbuzi tutawapata ili wananchi wetu waweze kufaidika.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, katika Jimbo la Mtambile kuna kituo cha Mifugo, ambapo wataalamu wa mifugo wapo wakati wowote kwa niaba ya wanawake anaowawakilishi wa Wilaya ya Mkoani, akitumie vizuri kile kituo, atapata ushauri elekeze namna gani na bora ya ufugaji wa mbuzi wa kisasa wa maziwa.

Mhe. Spika: Maswali tumemaliza na nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

Waheshimiwa Wajumbe leo kama tulivyojipangia kabla mwisho wa shughuli zetu kwa leo ni kumalizika kwa masuala ambayo yamepangwa katika orodha ya shughuli za leo. Kabla ya kuahirisha kikao chetu hichi nimeombwa nitoe Tangazo kwa waheshimiwa wajumbe wanawake.

Tangazo

Waheshimiwa Wajumbe wanawake wote wanaombwa kubakia ndani ya ukumbi huu ili watakuwa na mkutano wao wa Jumuiya yao ya UWAWAZA ndani ya ukumbi huu. Kwa hivyo waheshimiwa wajumbe wanawake nyote mnaombwa mbakie mara baada ya kuahirisha kikao hichi. Mwisho wa tangazo.

Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa mashirikiano makubwa katika kipindi hichi ha masuali. Hapa ndio mwisho wa shughuli zetu kwa leo. Baada ya hapo basi sasa naahirisha Kikao hichi hadi siku ya Jumatatu, tarehe 24/10/2011, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 4:20 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 24/03/2011 Saa 3:00 za Asubuhi).